

14-Nuwn Saakinah Na Tanwiyn

Nuwn saakinah: Ni herufi ya nuwn ن isiyokuwa na *i'raab* ambayo huthibiti katika kutamkwa, kuandikwa, kusimama na katika kuunganisha.

Tanwiyn: Ni nuwn saakinah iliyoziidi inapatikana mwisho wa nomino kwa kutamkwa wakati wa kuunganisha na hutengamana na hiyo nomino wakati wa kuandika na kusimama.

Tofauti baina ya nuwn saakinah na tanwiyn:

Nuwn saakinah ن	Tanwiyn ة
<p>Inapatikana katikati ya neno na mwisho wa neno.</p> <p>فَسَيُنْغِضُونَ - وَلَيْنَ</p>	<p>Inapatikana mwisho wa neno pekee.</p> <p>وَكَيْلًا</p>
<p>Inapatikana katika nomino kitenzi au kihusishi.</p> <p>الْمُنْخَنِقَةُ - يُنْفِقُونَ - مِنْ</p>	<p>Inapatikana katika nomino pekee.</p> <p>جُنُودًا</p>
<p>Huthibiti katika kutamkwa na kuandikwa katika hali ya kusimama na kuunganisha</p> <p>وَمِمَّنْ حَوْلَكُمُ</p>	<p>Hutamkwa wakati wa kuungwa na haithibiti katika kuandikwa hali ya kusimama.</p> <p>عَلِيمٌ قَدِيرٌ</p> <p>Mfano unapounga swifah mbili hizo za Allaah (سبحانه وتعالى), utasoma: عَلِيمٌ قَدِيرٌ. Na ukisimama katika عَلِيمٌ haitakiwi kusomwa عَلِيمٌ bali iwe عَلِيمٌ.</p>

Hukmu za Nuwn Saakinah na Tanwiyn

